# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

# TANGAZO

## MABADILIKO YA TAREHE YA KURIPOTI CHUONI KWA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA NA OFISI YA RAIS-TAMISEMI KUJIUNGA NA CHUO CHA USTAWI WA JAMII (KAMPASI YA DAR ES SALAAM NA KAMPASI YA KISANGARA) KATIKA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Chuo cha Ustawi wa Jamii kinawafahamisha wanafunzi wote waliochaguliwa na Ofisi ya Rais -TAMISEMI kujiunga na programu mbalimbali katika ngazi ya Stashahada ya Kawaida (Ordinary Diploma programmes) kwa mwaka wa masomo 2025/2026 kuwa wanatakiwa kuripoti Chuoni ifikapo tarehe 3 Novemba, 2025 badala ya tarehe 20 Oktoba, 2025 kama ilivyotangazwa hapo awali. Aidha, wanafunzi wote wanaweza kupata barua zao za maelekezo ya kujiunga na Chuo (Joining Instructions Letters) kupitia tovuti ya Chuo www.isw.ac.tz au wanaweza kupiga simu kupitia namba hizi: 0677 111200 au 0735509090 (Kampasi ya Dar es Salaam) na 0716121096 (Kampasi ya Kisangara) au wanaweza kufika moja kwa moja Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Dar es Salaam, eneo la Kijitonyama, au Kampasi ya Kisangara, iliyopo Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro.

**Limetolewa na**

**MKUU WA CHUO**

**18.08.2025**